Taarifa kwa vyombo vya habari| 22 Februari 2022

Wananchi na Viongozi Wilayani Maswa wanashirikiana kuleta mabadiliko

22 Februari 2022, Maswa: Twaweza inashirikiana na Shirika la Kawiye Social Development Foundation (KASODEFO), mamlaka ya serikali za mitaa na wakazi wa Maswa kuimarisha ushirikiano kati ya wananchi na viongozi ili kuboresha huduma za jamii, kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa serikali za mitaa na kuboresha ushiriki wa wananchi.

Kwa kutumia mbinu inayojulikana kama uraghbishi, Twaweza na KASODEFO zilifanya kazi ya kuwabaini na kutoa mafunzo kwa mawakala wa mabadiliko ya jamii, kufanya utafiti shirikishi na makundi mbalimbali ndani ya jamii, kuandaa na kutekeleza mipangokazi ya pamoja kuyashughulikia masuala yaliyoibuliwa. Twaweza pia ilifanya utafiti wa kina ili kuelewa hali ya huduma na mazingira halisi ya wakazi wa Maswa.

Matokeo muhimu kutoka kwenye utafiti ni:

- Wakazi wa Maswa 2 kati ya 10 (23%) wamejiunga na kikundi cha kijamii.
- Wakazi 7 kati ya 10 hawana taarifa ya mikutano yoyote ya kijiji iliyofanyika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kwa wachache wanaofahamu mikutano hiyo, kati yao 78% wanasema wamehudhuria mikutano hiyo. Hata hivyo, majadiliano ya kina kwenye vikundi na mapitio ya rejesta za mahudhurio vinaonesha mahudhurio yako chini.
- Miongoni mwa wanaohudhuria mikutano, ni wachache tu (25%) ndio wanaridhika na mikutano hiyo, wengi hawaridhiki kwasababu hawaoni vipaumbele vyao vikishughulikiwa na pia kwasababu hawapati mrejesho kutoka kwa serikali za mitaa kuhusu masuala yaliyoibuliwa siku za nyuma.
- Wananchi wana uwezekano mkubwa wa kukutana/kuwasiliana na viongozi wa vijiji kuliko wabunge au watendaji wa kata. Hata hivyo, wakazi wa Maswa 2 kati ya 3 (66%) wanasema hawajawahi kukutana na mwenyekiti wao wa kijiji.
- Wakazi wa Maswa wanapendelea zaidi kuchangia maendeleo ya jamii kwa kutoa fedha (72%), nguvukazi (63%) na vifaa (65%) baadhi yao kwa kugomea kutoa kodi (9%) au kutoa mawazo (40%).
- Mamlaka za mitaa huko Maswa zinaripoti kuwa kuna uhaba wa wafanyakazi, waliopo hawathaminiwi na hawana rasilimali na nyenzo za kutosha kutekeleza majukumu yao.
- Wakazi wa Maswa 7 kati ya 10 wanaohudhuria mikutano (65%) waliripoti kuwa taarifa za mapato na matumizi husomwa wakati wa mikutano ya Halmashauri ya Kijiji.
- Wakazi wa Maswa 8 kati ya 10 (82%) hawaridhishwi na miundombinu, na 5 kati ya 10 (52%) hawafurahishwi na upatikanaji wa umeme huku 6 kati ya 10 (60%) wameridhika na huduma ya elimu. Wananchi wa Maswa wamegawanyika karibu sawa kuhusu kuridhishwa au kutoridhishwa na huduma za usafi wa mazingira.

Hadi sasa, utafiti shirikishi umekamilika na maeneo muhimu ya kipaumbele kwa jamii yamefikiwa muafaka.

Maji

- Mwandete, Igunya, Ilula, Funika, Kadoto, Gula, Matalambuli, Mwatumbe, Budekwa, Bushitala, Zabazaba: Hawana huduma ya maji
- Igunya: Wanahitaji josho la kuogeshea ng'ombe

- Masela: Wanahitaji bwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji

Miundombinu

- Mwabulimbu, Igunya, Mwakulilima, Funika, Matalambuli, Mwatumbe, Masela, Budekwa, Sulu, Bushitala, Stendi Mpya: miundombinu ya barabara
- Matalambuli, Mwatumbe, Mwamihanza: kuunganishiwa umeme

Afya

- Mwandete: upungufu wa wafanyakazi wa afya
- Mwabulimbu: nyumba kwa ajili ya wafanyakazi
- Mwakulilima, Funika, Kadoto, Budekwa, Bushitala, Buhungukila, Mwamihanza, Zabazaba: Zahanati
- Gula: hakuna wafanyakazi wa afya
- Sulu: Kupandisha hadhi zahanati kuwa kituo cha afya

Elimu

- Mwabulimbu, Mwamihanza, Zabazaba: Nyumba kwa ajili ya walimu wa shule ya msingi
- Masela: Hakuna shule ya msingi kijiji cha Isada

Mahitaji muhimu ya maisha – (hoja kuhusu njia nzuri za kujipatia riziki za maisha)

- Mwandete: Mikopo kwa wanawake na vijana
- Mwakulilima: gulio (soko la wazi)
- Ilula: soko dogo, upandishaji wa wanyama
- Kadoto, Gula, Buhungukila: mbinu za kilimo bora
- Stendi Mpya: Mitaji, elimu ya ujasiriamali
- Buhungukila: upandishaji wa wanayama

Uongozi – (masuala yanayopaswa kushughulikiwa na viongozi)

- Sulu: Kujenga upya ofisi ya Mtendaji wa kijiji
- Stendi Mpya: Kuna hofu ya kukosekana usalama

Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza, alisema *"Mpango huu unatukumbusha kwamba ili maendeleo yaweze kutokea, tunatakiwa kuwashirikisha wananchi na kuhakikisha wanashirikiana na viongozi wao. Wananchi na viongozi wanapoaminiana na kumuona mwingine kama mshirika, taarifa zinapotolewa kwa uwazi na kwa wakati, na wote wakiwa na hamasa, ari, uwezo na fursa za kufanya kazi pamoja, matokeo yake ni mafanikio ya wazi na ya haraka."*

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi wasiliana na: Annastazia Rugaba | e: arugaba@twaweza.org | t: (+255)(0)687 22 197

Maelezo kwa Wahariri

- Twaweza inafanya kazi kupitia tafiti, ushahidi na kuchua hatua ili kuonesha jinsi ambavyo wananchi wanavyoweza kushirikiana kutatua matatizo yao na kuifanya serikali iwajibike vizuri zaidi kwa wananchi; kuwezesha wananchi kupaza sauti zao kwenye masuala yanayohusu maslahi na uzoefu wao ili yasikilizwe na yachukuliwe kwa uzito wakati wa kufanya maamuzi; na inahimiza kuweka mazingira wezeshi kwa ushirikishwaji wa wananchi na serikali kuitikia mahitaji ya wananchi nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Tufuatilie kwenye Twaweza Tanzania (Facebook), @Twaweza_NiSisi (Twitter), Twaweza East Africa (Instagram).